**HOJA BINAFSI YA MHESHIMIWA SULEIMAN MASOUD NCHAMBI (MBUNGE WA KISHAPU) KUHUSU UZALISHAJI NA UNUNUZI WA ZAO LA PAMBA NCHINI**

***(Chini ya Kanuni ya 54 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016)***

**Mheshimiwa Spika,**kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na tatizo kubwa kwenye uzalishaji na uuzaji wa zao la Pamba nchini hususani kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Bei ya pamba kuwa ya chini;

(b) Kila Mwaka kiwango cha pamba inayolimwa nchini kuporomoka;

(c) Ubora wa pamba kushuka kila Mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni miongoni mwa majawabu ambayo nimeyafanyia kazi kwa kina na kugundua ni sehemu gani tunakosea, na naomba niainishe maeneo yafuatayo:-

(a) Ikumbukwe zao la pamba halilimwi nchini pekee, zipo nchi lukuki duniani ambazo zinalima pamba kama vile India, China, Agentina, Brazil, Afrika ya Kusinin.k na karibu nchi zote hizo msimu wa kulima pamba unafanana kwa kiasi kikubwa ambapo huvunwa katika kipindi cha mwezi Juni na kuendelea;

(b) Pamba inayolimwa hapa nchini kwa kiwango kikukbwa huuzwa nje ya nchi ikiwabidhaa ghafi (*raw material*) badala ya kuitumia yote kiwandani na kuifanya kuwa zao la mwisho (*final product*);

(c) **Mheshimiwa Spika,** wakati wanunuzi wa nje ya nchi tunakouza pamba yetu hupenda kufanya mikataba mapema na nchi ambazo ziko tayari kuwauzia pamba, ni wakati huo wakulima wa Tanzania huwa wanasubiri kwanza kufunga mikataba hiyo mpaka pale wanapopata bei elekezi kutoka Bodi ya Pamba ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo;

(d) **Mheshimiwa Spika,** wakati mwingine Wakulima wa pamba nchini hulazimika kusubiri hadi katikati ya mwezi Juni au mwezi julai ili kupata bei hiyo elekezi na baadae kuingia mikataba na wafanyabiashara wa ndani kwa ajili ya kuuza pamba hiyo. Wakati huo huo wanunuzi wanamahitaji tayari ya bidhaa hiyo na hivyo kuwafanya kwenda nchi nyingine ambazo pamba inapatikana kwa wakati huo kwa sababu baadhi ya nchi Wakulima wake hawalazimiki kusubiri bei elekezi kutoka katika Serikali zao;

(e) **Mheshimiwa Spika,**kwa hiyo wafanyabiashara wanaouza pamba hiyo nje ya nchi wanakutana na changamoto ya wanunuzi wa nje ya nchi wakiwa tayari wameshanunua pamba kutoka nchi zingine ambazo zimewauzia mapema kwa ajili ya kulisha viwanda vyao na hivyo pamba yetu hununuliwa kama nyongeza tu.

Hivyo matokeo ya ucheleweshaji huu wa msimu yanawaathiri wakulima nchini moja kwa moja kwa sababu bei itakayouzwa pamba hiyo nje ya nchi iko chini na wafanyabiashara wa ndani nao watanunua kwa bei ya chini zaidi ili waweze kutengeneza faida;

(f) **Mheshimiwa Spika,**ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ni kuharakisha msimu wa pamba mapema ili wafanyabishara nchini wafunge mikataba hiyo mapema ambapo mahitaji yanakuwa yako juu na wanunuzi wa nje watakuwa badohawajanunua pamba nchi nyingine;

(g) **Mheshimiwa Spika,**kama kilo moja ya pamba itauzwa kati ya shilingi 1,500 – 2,000/= kuanzia mwezi Mei badala ya kati ya shilingi 600 – 1,200/= kati ya mwezi Julai na Oktoba. Faida zinazopatikana kwa kuharakisha msimu ni hizi zifuatazo:-

(i) Mkulima atapata kipato kikubwa na kwa wakati kwa kuuza pamba yake kwa bei ya juu;

(ii) Serikali itaongeza kipato kwa kukusanya kodi kwa kiwango kikubwa;

(iii) Ongezeko la bidhaa ya pamba kila mwaka kwa kuwa bei itashawishi Wakulima wengi kujiingiza kwenye kilimo cha zao la pamba baada ya kuona manufaa ya zao hilo;

(iv) Ongezeko la ajira kutokana na watu kujiajiri kupitia zao la pamba na hivyo kuweza kupunguza tatizo la ajira nchini;

(v) Serikali itaongeza kipato cha fedha za kigeni kwa kuuza zao la pamba nje ya nchi, ambapo fedha hizo zitaongezeka kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na hayo yapo matatizo mengine ambayo athari zake ni kubwa na zinamgusa mkulima wa pamba na Serikali moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,**Wakulima wa pamba nchini, wengi wao ni watu wa hali duni ambapo wanavuna pamba kati ya tarehe 1 Aprili na 15 Julai na hawana sehemu ya kwenda kuhifadhi pamba yao kutokana na kuwa na makazi finyu ambayo huyatumia na huwatosheleza tu kwa ajili ya maisha yao ya kila siku. Wakulima hao hawana uwezo wa kujenga nyumba ama hifadhi kwa ajili ya zao la pamba kutokana na kuwa maskini na kukosa kipato cha kujitosheleza.

**Mheshimiwa Spika,** mambo yafuatayo ni matokeo ya moja kwa moja pale mkulima wa pamba nchini anapochelewa kuuza pamba yake:-

(a) Anauza pamba hiyo kwa walanguzi wenzake katika Vijiji, Kata ama Wilaya anayoishi;

(b) Anauza kwa bei ya chini zaidi ili aweze kukidhi baadhi ya mahitaji yake ya kijamii na kiuchumi, kama vile:-

(i) Kusomesha watoto;

(ii) Matibabu;

(iii) Ununuzi wa chakula kwa ajili ya kujikimu na familia yake;

(iv) Dharura yeyote inapotokea; na

(v) Kulipa madeni kama vile madawa kwa ajili ya kustawisha na kuitunza pamba yake, kwani kipato chake ni sawa na Mtumishi ambaye

anapokea mshahara kati ya tarehe 29 na 30 katika kila mwezi. Lakini kwa mkulima wa pamba analima mwezi Novemba, anavuna mwezi Aprili na kusubiria mpaka mwezi Julai ili aweze kuuza pamba hiyo. Kwa hiyo mkulima anakaa na bidhaa hiyo ndani kwake kwa takribani miezi bila kuiuza.

(c) Kushuka kwa ubora wa bidhaa ya zao la pamba kutokana na kuwa baada ya kuvuna hakuna sehemu ambayo pamba hiyo inaweza kuhifadhiwa kitaalam ambapo mara nyingi huhifadhi pamba hiyo kwenye mazizi ya ng'ombeau juu ya ardhi mashambani na matokeo yake :-

- Pamba hiyo kubadilika rangi yake ya asili kutoka kuwa nyeupe hadi nyekundu;
- Kuchanganyikana na vumbi na mchanga;
- Kupigwa na jua kwa kiwango kisichostahili na kusababisha kupungua kwa ubora wake pindi inapotengenezwa kuwa nyuzi, na mbegu kupungua ubora wakati wa kukamuliwa mafuta.

(d) Ipo mifano katika miaka ya nyuma ikiwemo mwaka 2013 ambapo bidhaa ya pamba kutoka nchini ilikataliwa nje ya nchi na kurudishwa nchini jambo ambalo limewaletea hasara kubwa sana wanunuzi wa pamba nchini, na matokeo yake kama nchi jambo hili likatutia doa sana kwa kuuza pamba isiyo na ubora.

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa sababu hizo na nyingine nyingi zilizonisukuma nikuombe kwa idhini yako kuwasilisha hoja binafsi kwa mujibu wa Kanuni

ya 54 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016 niwasilishe hoja binafsi mbele ya Bunge lako tukufu kuhusu kuuangalia upya msimu wa pamba nchini kama ifuatavyo:-

**Kwa kuwa,** zao la pamba halilimwi nchini pekee, zipo nchini lukuki duniani ambazo zinalima pamba kama vile India, China, Agentina, Afrika ya Kusini na Barazil, na karibu nchi zote hizo msimu wa kulima pamba unafanana kwa kiasi kikubwa ambapo pamba huvunwa katika kipindi cha miezi ya Juni na kuendelea;

**Na kwa kuwa,** wakati huo wanunuzi hupenda kufanya mikataba mapema na nchi ambazo ziko tayari kuwauzia pamba;

**Na kwa kuwa,**Wakulima wa Tanzania husubiri kwanza kufunga mikataba hiyo mpaka baada ya kupata bei elekezi kutoka Bodi ya Pamba ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo;

**Na kwa kuwa,** zao la pamba linalimwa nchini wakatinchi yetu haijawa tayari kuifanya kama bidhaa ( *Final product*) na badala yake kwa kiwango kikubwa huuzwa nje ya nchi ikiwa ghafi *(raw material*);

**Na kwa kuwa,** jawabu la moja kwa moja la kuondokana na changamoto hizo kwa Wakulima wa pamba nchini ni kuharakisha msimu mapema wafanyabishara wafunge uuzaji wa mikataba hiyo mapema ambapo mahitaji yanakuwa yako juu na wanunuzi wa nje hawajanunua pamba nchi nyingine;

**Hivyo basi** ,mimi Suleiman Masoud Nchambi, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, naomba Bunge lako tukufu liniunge mkono katika hoja

yangu na kuazimiakuitaka Serikali ibadilishe msimu wa pamba kwakuanza msimu tarehe 1 mwezi Mei badala ya kufungua msimu kuanzia katikati ya mwezi Juni ili kuendana na hali halisi ya msimu wa uzalishaji na uuzaji wa pamba nchini. Hali hiiitapelekea kuendana na misimu ya pamba katika nchi nyingine zinazolima pamba duniani na hatimaye kuwa na uwezo wa kuuza pamba hiyo kwa bei nzuri kama wafanyavyo wafanyabiashara wa nchi nyingine duniani.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja

Mhe. Suleiman Masoud Nchambi

**MBUNGE WA JIMBO LA KISHAPU**